



# Kutengeneza unga wa samaki na dagaa kamba

## Kuongeza thamani

Kuongeza thamani ni changamoto kubwa kwa wavuvi wadogowadogo, wafuga samaki, wafanya biashara, na wachakataji, hasa wale walio katika nchi zinazoendelea. Kuongeza thamani katika samaki huongeza muda wa kuwahifadhi, hupunguza upotevu baada ya kuwavua, husaidia kukabiliana na mahitaji yanayobadilika na ladha mpya kwa wateja, na vile vile kuongeza upatikanaji wa masoko. Kuna njia mbalimbali za kuongeza thamani katika samaki. Kutengeneza unga wa samaki kutokana na samaki waliokaushwa ni njia ambayo kwa kiasi fulani haijaoeleka sana katika kuongeza thamani ambayo inaweza kusaidia kupenya katika soko linalolipa pesa nyingi zaidi, kwa mfano, maduka makubwa. Unga wa samaki ni rahisi kuu-fungasha na kuusambaza na unahifadhika kwa muda mrefu.



©FAO/Samuel Creppy

## Vifaa vya muhimu


Kutengeneza unga wa samaki kunaweza kufanywa kwa kutumia vifaa visivyo vya gharama. Vifaa vya msingi vina- vyohitajika ni oveni, kinu na mchi au kisagio, visu, vijiko, chekeche, mizani, vifungashio na lebo ili kufungasha bidhaa iliyo tayari. Uchakataji wa kutengeneza unga wa samaki unaweza kukamilishwa ndani ya siku moja.

## Hatua muhimu

Kwanza, nunua samaki au dagaa kamba waliokaushwa kwa moshi au njia nyingineyo kutoka sokoni na watunze kati- ka hali ya usafi na kuwafunika vizuri. Baadhi ya bidhaa za samaki kama vile changu nchini Ghana ni rahisi kuwasaga na huwa na ladha nzuri wanapokuwa katika umbo la unga. Samaki husafishwa na kusagwa kuwa unga. Hii inaweza kufanyika katika mashine ya kusaga iliyo jirani. Chekecha unga wa samaki ili kupembua uchafu na kisha ubanike katika oveni kwa kama dakika 10 ili kuondoa unyevunyevu zaidi. Weka unga uliobanikwa katika eneo linalopitisha hewa ili upoe. Hakikisha makasha ni makavu kwani unyevunyevu wowote unaweza kuharibu. Pima unga kwa vipimo tofauti na kisha ufungashe katika mifumo ya plastiki, funika, weka rakili na bandika lebo yako.

## Kutafuta masoko kwa ajili ya unga wa samaki

Kuongeza thamani kwenye bidhaa zako kunaweza kuwa rahisi baada ya kujua soko na fursa zinazokuzunguka. Tafiti njia mpya na rahisi za kufanya kazi na tenga muda na rasilimali kwa ajili hiyo. Ufumbuzi unaou pata unaweza kukupatia kipato bora. Ukipata wateja sahihi uau moja kwa moja ama kupitia maduka ya jirani, unaweza kujijengea jina kwa bidhaa zako zenye ladha nzuri.



## Tazamo video

<https://youtu.be/9U1k1ExjShE>



Pitisha simu kwenye  
alama hii ili kutazama  
video